# Nafasi ya Lugha na Vyombo vingine vya Kimawasiliano katika Vita Dhidi ya UKIMWI Nchini Kenya

*Mosol Kandagor*

**Ikisiri**

Zaidi ya miongo mitatu iliyopita masuala ya UKIMWI[1] yalianza kuripotiwa ulimwenguni. UKIMWI ni mojawapo ya magonjwa ambayo hayana tiba na kwamba umeenea kwa kasi sana katika mataifa mbalimbali ulimwenguni. Mataifa mengi ulimwenguni yameendelea kutatizika kutokana na athari za ugonjwa huu. Kwa mfano, nchini Kenya UKIMWI umewaangamiza watu wengi, na kwa sasa ni janga la kitaifa; ugonjwa huo ulitangazwa kuwa janga la kitaifa mwaka 1999. Makala haya basi yanabainisha nafasi ya lugha na vyombo vingine vya kimawasiliano katika kukabiliana na UKIMWI. Aidha, makala yanajikita katika kuonyesha jinsi wahudumu wa Wizara ya Afya pamoja na wadau wengine wanavyoteua na kutumia istilahi maalumu katika harakati za kupunguza kuenea kwa ugonjwa huu ambao kwa hakika hukita mizizi kila uchao. Utafiti huu ulifanywa katika taasisi mbalimbali zinazohusika na utafiti wa UKIMWI na pia wagonjwa wenyewe kwa kutathmini nafasi ya lugha katika harakati zao za kukabiliana na ugonjwa huo. Data zilizochanganuliwa zilikusanywa kutoka kituo cha AMPATH[2]-Eldoret, mabango, vyombo vya habari na maandishi mengine yanayobeba maelezo juu ya kupunguza kuenea kwa UKIMWI.

## 1.0 Utangulizi

Katika karne hii ya ishirini na moja kuna mambo mengi ambayo yamewatatiza binadamu kwa namna moja ama nyingine. Matatizo hayo yumkini yamesababisha kuwapo kwa hali ya wasiwasi mwingi miongoni mwa binadamu. Wasiwasi huo umeibuka kuwa changamoto na kizingiti kikubwa katika maisha na maendeleo ya watu kote duniani. UKIMWI ni mojawapo ya janga ambalo limesababisha kuwapo kwa wasiwasi na matatizo ambayo yameibuka kuwa changamoto katika karne hii. Mbali na UKIMWI, uchumi, masuala ya kiutamaduni, elimu na hali ya maisha kwa jumla imesababisha kuwapo kwa hali ya wasiwasi miongoni mwa binadamu. Tukitazama kwa makini, vipengele hivi ni baadhi ya mambo ambayo yameendelea kuwatatiza binadamu katika enzi hizi za utandawazi. Simala (2008: 64-65) anadai kuwa:

---

[1] Upungufu wa Kinga Mwilini

[2] Academic Model Providing Access to Health Care

> Dhana ya utandawazi imeathiri ulimwengu na inaendelea kuubadilisha kwa njia kuu. Baadhi ya watu wanahisi kuwa utandawazi umejitokeza kuwa nadharia kuu ya ulimwengu ambayo inatawala kila hali ya maisha. Hakuna asasi wala taaluma moja ambayo haijashuhudia mabadiliko hayo. Awali mfumko wa utandawazi ulisababisha wasiwasi miongoni mwa wanataaluma mbalimbali. Watu wengi walihofia hatima ya taaluma zao kutokana na athari za utandawazi. Hali hiyo ilitokana na kutokuwa na uhakika kuhusu mwelekeo wa matukio mengi yenye vishindo. Utandawazi unatoa changamoto kubwa sana kwa taaluma. Kote ulimwenguni, taaluma mbalimbali zinahitaji kuwashirikisha wahusika wote katika kuielewa hali yenyewe, pamoja na athari zake.

Kutokana na maelezo hayo ni bayana kuwa utandawazi umeathiri kila uwanja wa maisha ya binadamu. Athari hizo zinatokana na sababu kuwa, kuna maendeleo makubwa ya kiteknolojia katika nyanja mbalimbali. Katika karne hii ya ishirini na moja, binadamu hawana budi kwenda na kasi hiyo ya teknolojia ambayo imechochewa na msukumo wa utandawazi. Kutokana na hali hiyo basi ni muhimu kubainisha mbinu zinazotumika katika kukabiliana na vita dhidi ya UKIMWI. Lugha ni kifaa muhimu sana ambacho huweza kutumika kupiga vita kuenea kwa UKIMWI. Lengo kuu la lugha ni kuhakikisha kuwa binadamu wanawasiliana. Katika mkabala huo, lugha huweza kutumika kuwasilisha habari au maelezo ambayo yanaweza kusaidia katika kukabiliana na vita hivi vikali dhidi ya UKIMWI.

## 2.0 Lugha na UKIMWI

Lugha hutumiwa hasa na binadamu katika kutekeleza shughuli mbalimbali. Kimsingi lugha hueleweka kama chombo cha mawasiliano. O’grady na wenzake (1997), Ogechi (2002), na Habwe na Karanja (2004) wanakubaliana kwamba lugha ni mfumo wa sauti, ishara na maandishi unaotumika kama chombo cha kuwasilisha habari kwa wanajamii husika; kwamba binadamu hutumia lugha kupashana habari, kufafanua dhana au hata kutoa mwelekeo kuhusu suala fulani katika jamii. Kutokana na maelezo hayo, tunaweza kudai kuwa lugha ina nafasi maalumu na muhimu katika vita dhidi ya UKIMWI. Hayo yote hufanyika kupitia mbinu na mikakati anuwai ambayo imewekwa ili kuwasilisha ujumbe mbalimbali unaobeba maandishi au picha zinazoeleza juu ya njia za kujiepusha au kupiga vita ugonjwa huu. Kipengele kinachoelekea kuchomozwa hapa ni mawasiliano.

Kimsingi mawasiliano ni hali ya kupitisha habari au ujumbe kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Aghalabu mawasiliano huhusisha watu wawili au zaidi, hata hivyo kuna uwezekano wa kuwa na mawasiliano yanayojumuisha mtu mmoja pekee. Sharma (2008) anadai kuwa mawasiliano ni hali ya kutoa habari kutoka

kwa mtu *A* hadi mtu *B*, au sehemu *A* hadi *B* kwa kuhusisha njia fulani maalumu. Pia anaendelea kusema kwamba mawasiliano ni njia fulani inayoweza kuwaleta watu pamoja. Watu hao wanapokuja pamoja wanaweza kutagusana, na mitagusano yao husababisha athari ambazo zinaweza kuwa chanya au hasi. Katika mawasiliano yoyote yale, kwa mfano yanayohusu janga la UKIMWI, inatarajiwa kwamba kuna mtoaji habari kwa upande mmoja na mpokeaji habari kwa upande mwingine. Anayepokea habari ni mwathirika ilhali anayetoa habari katika muktadha wetu ni Wizara ya Afya, kituo cha AMPATH na wahusika wengine.

Taylor na wenzake (1980) wanadai kuwa mawasiliano ni kipengele muhimu sana katika maisha ya binadamu, kwani humwezesha kutangamana na ulimwengu. Aidha, ni njia pekee ya kujua kinachotendeka kote ulimwenguni. Aghalabu binadamu wanapowasiliana hufanya hivyo kwa makusudi au bila kukusudia. Vile vile, mawasiliano huweza kutazamwa kihatua; kwamba, kuna hatua zinazozingatiwa katika mawasiliano. Yaani kwanza utambue unachotaka kuwasilisha, kisha unawasilisha kwa nani, halafu unawasilisha kwa sababu gani. Pia ni muhimu kutambua kwamba tunapowasilisha ujumbe, tunafanya hivyo kwa ruwaza maalumu, yaani kwa kuzingatia hatua maalumu. Hatua na vipengele hivi vyote huzingatiwa katika kutoa habari na maelezo yanayohusiana na UKIMWI. Ogechi (2002:2) anadokeza kuwa:

> Inaelekea kwamba mawasiliano yanahitaji mambo kadha: ujumbe/habari, usafirishaji, nyenzo/njia, mtuma-ujumbe na mpokeaji-ujumbe. Kwa hivyo, tunaweza kutoa kijelezi chetu kuwa: Mawasiliano ni usafirishaji wa ujumbe kutoka kwa mtuma-ujumbe hadi kwa mpokea-ujumbe kwa kutumia nyenzo fulani. Aidha, ujumbe unaweza kuwasilishwa kwa kutumia nyenzo kadha. Nyenzo hizo ni pamoja na: ngoma, miondoko ya mwili, picha na/au michoro, na lugha.

Maelezo ya Ogechi yanatuelekeza kwa kipengele muhimu sana, yaani nyenzo za mawasiliano. Nyenzo inaweza kuelezwa kama namna au njia ya kuwasilisha kitu fulani kama vile habari na ujumbe. Nyenzo hizo ni kama kivuko kinachotusaidia kuvusha ujumbe kutoka kwa anayetoa habari kwa upande mmoja, hadi yule anayepokea kwa upande mwingine. Katika muktadha wetu nyenzo hizo ni picha, mabango, pamoja na maandishi mbalimbali ambayo yanatumiwa katika vita dhidi ya UKIMWI. Pia, mawasiliano hukua na kuboreshwa kila uchao. Mawasiliano hupitia hatua za mabadiliko kutegemea wakati au kipindi kinachohusika; kwa mfano, awali mawasiliano juu ya UKIMWI na athari zake yaliwekwa kuwa siri. Yalijulikana tu miongoni mwa mgonjwa na daktari au muuguzi pekee au

ndugu wa karibu. Hata hivyo hali hiyo imebadilika, katika karne hii ya ishirini na moja wanaougua ugonjwa huo wanahimizwa kujitokeza wazi bila hofu yoyote ili waweze kusaidiwa.

Taylor na wenzake (1980) na Ogechi (2002) wanadokeza kuwa, dhana ya elementi za mawasiliano ni mambo muhimu ambayo lazima yawepo katika mawasiliano. Elementi hizo ni pamoja na: chanzo cha ujumbe, mpokeaji ujumbe, ujumbe na njia za kusafirisha ujumbe unaohusika. Wanaendelea kudai kuwa wakati na mahali pa mawasiliano huathiriwa na wahusika, mapambo, idadi ya watu na mavazi miongoni mwa mengine. Kuhusu mawasiliano yanayodhamiriwa kuchangia katika vita dhidi ya UKIMWI, si lazima elementi hizo zijitokeze. Kilicho muhimu ni namna ya kuwasilisha ujumbe na vifaa vinavyotumika katika mawasiliano. Kwa mfano, matumizi ya picha, mabango na matangazo ambayo yanaweza kujitokeza kiusemi, kielektroniki na hata kimaandishi.

Mawasiliano pia hutegemea masuala ya kiutamaduni. Taylor na wenzake (1980) wanadai kuwa utamaduni ni jumla ya maisha ya watu ambayo hujengwa na kikundi cha watu na kusambazwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Utamaduni huibua lugha, tabia, ishara na maana zinazotokana na mambo fulani. Katika jamii tunajifunza kutambua ni maneno gani tunaweza kutumia katika mawasiliano, ishara zipi zitatumika, jinsi ya kunena na maneno yapi yanafaa kuteuliwa na kutumika katika mawasiliano mbalimbali. Haya yote yanatendeka katika jamii ikichukuliwa kwamba kila jamii ina namna yake ya kutenda na kutekeleza mambo mbalimbali. Katika msingi huo wa utofauti katika masuala ya kiutamaduni, tunaweza kudai kuwa hiyo ndiyo sababu ya kila kikundi cha watu kuwasiliana kwa namna tofauti tofauti (Kandagor, 2000). Kila jamii ina namna yake ya kutumia lugha inayofaa katika muktadha unaohusika ili kuwasilisha habari inayofaa kwa jamii inayolengwa (Kutol, Kandagor na Simotwo, 2009). Katika mkabala huo Wizara ya Afya imesaidia sana katika kusambaza maelezo yanayokusudiwa kupunguza kuenea kwa UKIMWI kwa lugha zinazoeleweka na jamii inayolengwa kutegemea hali ya utamaduni wao. Kwa jinsi hiyo, mbali na kutumia Kiswahili, Wizara ya Afya pia imejaribu kutafsiri maelezo muhimu kwa takriban lugha zote nchini Kenya[3], hasa katika maeneo yanayoaminika kuwa ugonjwa huo hatari umeenea sana (Treichler, 1989 na *New York Times*, 2004).

[3] Baadhi ya lugha hizo ni: Kikikuyu, Kinandi, Kimeru, Kikamba, na Kigiriama. Kwa jumla, kuna makabila arobaini na mbili katika taifa la Kenya.

**3.0 Ugonjwa wa UKIMWI**

Kimsingi UKIMWI ni akronimu inayorejelea Upungufu wa Kinga Mwilini. Ni ugonjwa ambao umewatatiza na kuwaathiri watu wengi sana; wagonjwa, wasio wagonjwa, wanasayansi na wanajamii kwa jumla. Kwa sasa UKIMWI huchukuliwa kama janga la kitaifa, siyo tu katika taifa la Kenya bali pia kote ulimwenguni. Githaiga na wenzake (2008) wanaeleza kuwa UKIMWI ni ugonjwa hatari sana kwa jamii kwani umewaathiri watu wengi sana katika taifa la Kenya. Wanaendelea kusema kuwa ni kutokana na hali hiyo ndipo Rais wa pili nchini Kenya Daniel Toroich Arap Moi akatangaza UKIMWI kuwa janga la kitaifa katika mwaka 1999. UKIMWI ulianza kuripotiwa kwa mara ya kwanza mwaka 1981 kule Marekani miongoni mwa wanaume mashoga waliojulikana maarufu kama *Gay-men*, na ugonjwa wenyewe ukifahamika kama GRID[4].

Hata hivyo, baadaye wanasayansi walibainisha kuwa visa vya virusi vya UKIMWI vilikuwapo kabla ya 1981. Katika misingi hiyo wanadai kuwa katika mwaka 1959 mwanamume mwenye asili ya Kibantu kutoka nchi ya Ubelgiji alihofiwa kufa nchini Kongo kutokana na ugonjwa wa UKIMWI baada ya Vita Kuu vya Pili vya Dunia. Tangu ulipogunduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1981, UKIMWI umewaua takriban watu milioni ishirini na tano. Kwa sasa inadaiwa kuwa umeenea sana katika mataifa ya India, Indonesia, Papua New Guinea, Vietnam, Ukraine, Estonia na Latvia (Kunhiyop, 2008).

Wain (2005) katika makala yake (*1959 and all that-Immunodeficiency virus*) anadai kuwa ingawa kumekuwapo na mtafaruku wa chanzo cha UKIMWI, hakuna uhakika kuwa ugonjwa huo ulianzia Afrika. Anaendelea kudai kuwa wanasayansi wengi wanaoamini kuwa UKIMWI ulianzia katika bara la Afrika wanatumia kigezo kisichokuwa na msingi maalumu. Madai hayo yamekitwa katika udunishwaji wa Bara la Afrika pengine kwa sababu ya hali mbovu ya kiuchumi na umaskini ambao umekita mizizi barani.

**4.0 Lugha katika Vita dhidi ya UKIMWI**

Data zilizokusanywa na kuchanganuliwa katika utafiti huu zimeainishwa na kuchanganuliwa katika misingi mikuu mitatu. Tumeziainisha data zetu kulingana na njia iliyotumika kuwasilisha habari husika. Kwa jinsi hiyo, tumeibuka na kategoria kuu tatu ambazo ni matini za kimaongezi, kimaandishi na kielektroniki.

[4] Gay-related immune deficiency

### 4.1 Mawasiliano ya Maongezi katika Vita dhidi ya Ukimwi

Katika kategoria hii tumechanganua data zilizotolewa moja kwa moja kimaongezi kwa wagonjwa wa UKIMWI na hata wale wasiokuwa wagonjwa. Halikadhalika, maelezo yaliyoainishwa katika kategoria hii ni pamoja na maelezo ya moja kwa moja ya madaktari kwa wagonjwa, wanasiasa, mafundisho ya kidini na ushauri nasaha na kupima kwa hiari (VCT)[5] katika kituo cha AMPATH. Tuangalie basi lugha hiyo inavyojitokeza katika asasi na wadau hao mbalimbali.

#### 4.1.1 Lugha ya Vituo vya Afya

Vituo vya afya viko mstari wa mbele kutoa huduma za afya ikiwemo ushauri nasaha na vipimo. Ushauri nasaha hutolewa kwa watu wote juu ya athari za UKIMWI. Ushauri huu hutolewa kwa hiari bila malipo yoyote. Ushauri na upimwaji wa kujua hali ya mtu ya maambukizi hufanywa katika vituo mbalimbali nchini Kenya (CDC[6], 2008). Watu wa matabaka mbalimbali hushauriwa kutembelea vituo hivyo ili kujua afya zao bila kujali kama wana UKIMWI au la. Mbali na kutoa ushauri, vituo hivyo huwaelimisha watu kuhusu hatari za UKIMWI na umuhimu wa kujua hali zao na hata jinsi ya kuepukana na virusi hivyo. Baada ya maelezo muhimu ama kwa mtu binafsi au kwa umma, uamuzi wa kupimwa au kutopimwa ni hiari ya mtu binafsi. Matokeo ya kupimwa huwa siri kati ya mpimaji na anayepimwa. Katika kutekeleza shughuli hiyo, istilahi au kauli maalumu hutumika katika mawasiliano. Tazama mifano ifuatayo:

**a) ABC**[7]

Hii ni akronimu maarufu inayotumika katika ushauri wa jinsi ya kuepukana na UKIMWI. Kila herufi katika akronimu hii ina maana yake; husimamia hatua mojawapo katika kupigana vita dhidi ya UKIMWI. Herufi *A* inasimamia neno *Abstain* lenye maana ya kujiepusha kufanya ngono, *B* inasimamia *Be Faithful*, yaani kuwa mwaminifu kwa mpenzi, mke au mume mmoja. Kwa upande mwingine *C* inasimamia *Condom*; yaani ukishindwa hatua *A* na *B*, basi unaweza kutumia kondomu zilizoidhinishwa na WHO[8] wakati wa kufanya mapenzi. Kwa kiasi kikubwa hatua hizi tatu zimesaidia sana katika kukabiliana na janga hili la UKIMWI kote ulimwenguni.

**b) Tumia Kifaa Kimoja wakati wa Tohara**

---

[5] Voluntary Counseling and Testing
[6] Centre for Disease Control
[7] Abstain Be faithfull or use Condom
[8] Word Health Organization [Shirika la Afya Duniani]

Ngariba hushauriwa kuwa makini wakati wa kutekeleza tendo hili (tohara) la kitamaduni. Kwamba, wakati wavulana wametimiza umri wa kutahiriwa, ngariba lazima atumie vifaa tofauti kwa kila mmoja anayemtahiri, la sivyo anaweza kusambaza UKIMWI kwa makusudi au hata bila kukusudia. Nilipowahoji baadhi ya madaktari, wauguzi na watu mbalimbali juu ya hatua hii, walisema kuwa ngariba akiizingatia njia hii ipasavyo anaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika vita dhidi ya kuenea kwa UKIMWI.

**c) Kula Lishe Bora**

Watu ambao wameambukizwa virusi vya UKIMWI hushauriwa kula vyakula bora. Wanahimizwa kula kulingana na mwongozo wa lishe bora ambao umeidhinishwa na wataalamu wanaohusika na masuala haya. Kwa mfano, wanapaswa kula vyakula vyenye madini, vitamini, wanga, mafuta na vyakula vingine ambavyo vinaweza kuongeza uwezo mwilini wa kukabiliana na virusi ambavyo tayari viko mwilini. Katika kutekeleza wajibu huu kituo cha AMPATH-Eldoret kimeanzisha mradi wa kupanda nafaka na kusambaza mavuno kwa waathirika wa UKIMWI katika mji wa Eldoret na maeneo mengine ambapo shirika la AMPATH lina kliniki.

**d) Hudhuria Kliniki Kulingana na Ratiba**

Katika kituo cha AMPATH-Eldoret, watu walio na virusi hushauriwa kuhudhuria vikao vya kliniki kulingana na ratiba waliyowekewa. Kwa mujibu wa kituo hicho, kila mgonjwa ana siku na saa yake maalumu ya kuhudhuria kikao chake ili kupata ushauri unaofaa. Pia wale ambao hawana uwezo wa kifedha hupewa nauli ili wasikose miadi yao. Kila wanapohudhuria miadi yao, hukumbushwa na wauguzi na madaktari kuhakikisha kuwa wanafika hospitalini kila wanapohitajika kufanya hivyo, ili wapate ushauri wa kutosha juu ya kujiepusha na UKIMWI au maambukizi mapya.

**e) Tumia Dawa za Kupunguza Makali ya UKIMWI**

Watu wote ambao wana virusi vya UKIMWI hushauriwa kutumia dawa za kupunguza makali ya ugonjwa huo (ARVs)[9]. Kituo cha AMPATH-Eldoret na vituo vingine kote nchini Kenya hutoa dawa hizo kwa waathirika bila malipo yoyote.

### 4.1.2 Lugha ya Wanasiasa

Kwa kiasi kikubwa wanasiasa wamechangia katika kupiga vita ugonjwa wa UKIMWI. Wanasiasa wengi huchukua nafasi katika mikutano yao na wananchi kuwakumbusha kuwa UKIMWI ni hatari. Aghalabu, wanasiasa

[9] Anti-Retro-Virals

wanapoalikwa kuhutubia katika mikutano mbalimbali ya hadhara, huchukua nafasi hiyo kuwashauri watu kujiepusha na ugonjwa wa UKIMWI. Kwa mfano, mwaka 2006 Rais Mwai Kibaki pamoja na mkewe Lucy walijitokeza hadharani katika kituo cha Ushauri Nasaha na Kupima kupokea ushauri na pia kupimwa ili wajue afya zao. Kule kujitokeza wazi kwa kiongozi wa nchi ni ishara tosha kwamba kila mwananchi anapaswa kujua afya yake. Shughuli hiyo ilifanyika wakati wa kampeni ya kuwahamasisha watu juu ya umuhimu wa kujua hali zao za UKIMWI kama njia mwafaka ya kujikinga au kupunguza kuenea kwa virusi vya UKIMWI. Baadhi ya maneno yanayotumiwa na wanasiasa ni pamoja na *UKIMWI ni hatari, UKIMWI utawamaliza, Tumieni kondom (mipira) wakati wa mapenzi* na *UKIMWI hauna tiba*. Kwa namna moja au nyingine, tunaweza kudai kuwa juhudi za wanasiasa zimechangia kwa kiasi kikubwa katika vita dhidi ya ugonjwa huu wa UKIMWI.

### 4.1.3 Lugha ya Viongozi wa Dini

Dini ni mojawapo ya asasi muhimu katika au kueleza madhara au kupiga vita kuenea kwa maradhi mbalimbali, kama vile UKIMWI. Shirika la Afya Duniani na Wizara ya Afya Kenya zinatambua nafasi ya viongozi wa kidini katika vita dhidi ya UKIMWI. Hii ni kwa sababu viongozi wa dini huwa na umma mkubwa ambao ni wafuasi wao. Pia, inachukuliwa kwamba viongozi wa kidini hukutana na wafuasi wao mara kwa mara, kwa hivyo wana uwezo wa kutoa mafunzo yanayohusiana na UKIMWI kwa wafuasi husika (*Daily Nation* Mei 20, 2010). Ingawa hakuna njia na wakati maalumu wa kutoa mafunzo hayo, viongozi wa kidini hujitahidi wawezavyo kuwajuza wafuasi wao kila wanapopata nafasi ya kufanya hivyo madhabahuni.

Katika Biblia takatifu, kuna baadhi ya maneno ambayo yanawahimiza watu kuishi maisha ambayo yanaweza kupunguza kuenea kwa UKIMWI. Mathalani, *kunywa maji kutoka kisima chako* (Biblia Takatifu 1997, Methali 5:15), na *usizini na wala usitamani mke wa jirani yako* (Biblia Takatifu 1997, Kutoka 20:17). Ingawa maelezo hayo hayataji moja kwa moja kuhusu UKIMWI wachungaji wa dini ya Kikristo hutumia kama kigezo cha kupimia maisha ya Mkristo aliyekamilika na mwenye maadili mema, hasa katika masuala ya ngono. Baadhi ya wachungaji niliowahoji walidhihirisha matumizi ya maneno yafuatayo kama njia mojawapo ya kuwahimiza kujiepusha na ugonjwa wa UKIMWI: *Elfu moja na mia mbili*. Haya ni maelezo yanayotumika kurejelea sehemu ya siri ya mwanamume, kwa upande mwingine neno *kawagware* hutumika kurejelea sehemu ya siri ya mwanamke. Neno hili lina asili yake katika jamii ya Wakikuyu linalomaanisha *kwa Wangare* (jina la kike). Udondoshaji umetumika kuibuka na neno *kawangare*. Maelezo hayo ni tafsida na hukusudiwa kusaidia katika kukabiliana na janga

hili la UKIMWI. Mmoja wa wahubiri aliyekuwa akiwafundisha vijana juu ya kujiepusha na ngono kabla ya ndoa katika kanisa moja la Kiadventista mjini Eldoret alinukuliwa akisema:

1. *Vijana mjihadhari na safari za kawagware kwani mnaweza kumaliza pesa zenu elfu moja na mia mbili kwa walaghai wa mapenzi. Mkitaka kufaulu ziwekeni pesa zenu vizuri ili mzitumie kwenda kawagware wakati wake ukifika. Mkifanya hivyo mtapata faida kamili.*

2. *Wavulana msitumbukize mikono yenu kwa kila shimo kwani huwezi kujua kuna nini katika shimo hilo. Kuna mashimo mengine ambamo mnaweza kupata asali na mengine nyoka hatari wenye sumu kali. Kabla ya kutumbukiza mikono hakikisha umepata leseni kutoka kwa daktari na mchungaji.*

3. *UKIMWI ni shetani na huangamiza kama afanyavyo shetani.*

Katika mifano hii, tafsida (lugha yenye kuficha ukali wa maneno) imetumika kwa kiwango kikubwa. Mhubiri huyo alikuwa akizungumzia mapenzi kati wa wavulana na wasichana. Maelezo yake yalimaanisha kwamba mapenzi kati ya vijana ambao hawajafunga ndoa yanaweza kuwaharibia maisha yao ya baadaye kwa kuwa wanaweza kukumbana na nyoka wenye sumu kali, yaani UKIMWI. Pia vijana wanahimizwa kupata ushauri na kupimwa katika vituo vya ushauri nasaha na kupima ili kujua hali zao kabla ya kufunga ndoa. Baada ya kujua hali zao, wanaweza kumwona mchungaji ili aweze kuwaunganisha kama mke na mume.

### 4.1.4 Lugha ya Vijana

Vijana pia wamechangia sana katika vita dhidi ya UKIMWI. Ogechi (2005) anadai kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu hutumia istilahi teule katika kuonesha jinsi ugonjwa huo ulivyo hatari. Baadhi ya maneno hayo ni: *Mdudu, Kimbunga, Kamsaada-Aid, Ka-mdudu, Homa, Tsunami na Kupigwa-na-stima.* Maneno haya huibua hisia fulani miongoni mwa waathirika. Mfano, kimbunga huweza kumpotezea tumaini katika maisha, ilhali homa inaweza kumpa tumaini; kwamba anaweza kuendelea kuishi licha ya kuwa na ugonjwa wa UKIMWI. Ingawa wanafunzi hao wamechangia katika kuibua maneno yanayochangia katika kupunguza kuenea kwa UKIMWI, uchunguzi wa Ogechi (2005) ulibainisha kuwa wanafunzi wengi katika vyuo vikuu hupuuza umuhimu wa kujikinga na virusi vya UKIMWI licha ya kuwa na kiwango kikubwa cha elimu.

### 4.2 Mawasiliano ya Maandishi katika Vita dhidi ya UKIMWI

Katika sehemu hii maandishi na picha mbalimbali zinazotolewa katika vitabu, ilani kwa wagonjwa na kwa njia nyingine yoyote ile ziliainishwa na kuchanganuliwa. Maandishi na picha hizo zilipatikana katika kuta za ilani katika kituo cha AMPATH, mabango mbalimbali katika mji wa Eldoret na viunga vyake, mavazi na magazeti. Maandishi na picha mbalimbali zinazobeba habari juu ya ugonjwa wa UKIMWI huandaliwa na Wizara ya Afya Kenya kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani. Maandishi na picha hizo husambazwa katika taasisi za elimu, ofisi za serikali na hospitali zote nchini Kenya.

#### 4.2.1 Juhudi za Wachapishaji Vitabu na Asasi za Elimu ya Juu

Mashirika ya kuchapisha vitabu yamejitahidi na kuwa katika mstari wa mbele katika kuchapisha vitabu na matini maalumu zinazoshughulikia UKIMWI. Baadhi ya mashirika hayo ni KIE[10], Oxford, MacMilan na Jomo Kenyatta Foundation. KIE ni kitengo kimojawapo muhimu katika Wizara ya Elimu ambacho huhusika na uratibu, uchapishaji pamoja na usambazaji vitabu na vifaa vingine vinavyotumika katika kuwafunzia wanafunzi katika shule za msingi, upili na vyuo vya kati. Kwa mfano, mashirika ya Oxford na KIE yameandaa mafunzo ya UKIMWI katika silabasi ya vyuo vya kati katika somo la *Social Studies*[11] ambalo hufundishwa kwa Kiingereza.

#### 4.2.2 Juhudi za Wizara ya Afya na AMPATH

Kwa kushirikiana na vituo mbalimbali vya AMPATH, Wizara ya Afya nchini Kenya imejaribu kuwaelimisha wanajamii juu ya athari za UKIMWI. Katika kuwaelimisha wanajamii, asasi hizo zimeibuka na mabango na picha ambazo zinabeba habari juu ya ugonjwa huu. Habari hizo zimebeba maelezo muhimu juu ya kujiepusha na kudhibiti UKIMWI.

##### 4.2.2.1 Mabango, Picha na Vijitabu

Mabango yametumiwa sana kote nchini Kenya katika harakati za kuwahamasisha watu kupiga vita UKIMWI, mengi yakiwa katika lugha mama[12] kutegemea jamii inayolengwa. Mutembei (2009) anadai kuwa

---

[10] Kenya Institute of Education (Taasisi ya Elimu Kenya)
[11] Mastering PTE: Social Studies na Githaiga et.al. kimechapishwa na shirika la Oxford, 2008
[12] Lugha hizo ni kama vile: Kikuyu, Kimeru, Kimaasai, Kitugen, Ki-Ekegusi, Kiturkana, Kisabaot n.k.

mabango ni njia mojawapo na muhimu inayoweza kutumika katika vita dhidi ya UKIMWI. Kwamba, ujumbe unaoandikwa katika mabango unaweza kubadilisha tabia za watu, kwa mfano, kuwazuia watu kufanya mapenzi kiholela, na kwa jinsi hiyo wanaweza kujiepusha na UKIMWI. Katika utafiti ilibainika kuwa mabango mengi hubeba taarifa zifuatazo: *Badilika uishi, Chanukeni pamoja, Trust ni kiboko yao* na *Kondom ni kiboko yao.* Pia picha nyingi huonesha watu ambao wana virusi vya UKIMWI kwa upande mmoja, na watu wasio na virusi hivyo kwa upande mwingine. Kwa upande mwingine kuna vijitabu vingi ambavyo vimeandikwa na kusambazwa kote nchini Kenya ili visomwe na watu wote hasa waathirika wa UKIMWI. Katika kituo cha AMPATH-Eldoret kuna vijitabu kama vile *Mpangilio wa Kinga kwa Wanaoishi pamoja na Virusi vya UKIMWI* ambavyo huonesha hatua zifuatazo zinazopaswa kuzingatiwa na waathirika wa UKIMWI:

> ***Hatua ya kwanza:*** Wape wanaoishi na virusi vya UKIMWI ushauri wa kujikinga kila watembeleapo kliniki.
> ***Hatua ya Pili:***Chunguza jinsi anayeishi na virusi vya UKIMWI anavyofuata maagizo ya matumizi ya dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI pamoja na/au matibabu mengine kila anapokuja kliniki.
> ***Hatua ya Tatu:*** Chunguza anayeishi na virusi vya UKIMWI ikiwa ana ishara na dalili za magonjwa ya zinaa kila anapokuja kliniki.
> ***Hatua ya Nne:*** Chunguza hali ya mimba na nia za anayeishi/wanaoishi na virusi vya UKIMWI pamoja na za mpenzi/wapenzi wao kila anapo/wanapokuja kliniki.
> ***Hatua ya Tano:*** Mpe anayeishi na virusi vya UKIMWI mpira kila anapokuja kliniki.
> ***Hatua ya Sita***: Mwelekeze anayeishi na virusi vya UKIMWI kwa Mshauri kwa mjadala zaidi na/au huduma za jamii kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

### 4.3 Mawasiliano ya Kielektroniki katika Kukabiliana na UKIMWI

Katika sehemu hii data zilipatikana kutoka kwa vyombo vya kielektroniki kama vile runinga, redio na rununu. Mawasiliano kwa njia ya elektroniki au vyombo vya habari aghalabu huchukuliwa kufikia idadi kubwa ya watu. Katika vyombo vingi vya habari kuna matangazo ya biashara kama vile: *Kleptomaniax ana yake je una yako? Achana na mpango wa kando epuka UKIMWI, Chanukeni pamoja* na *tumechill.* Maelezo na matangazo haya

pamoja na mengine yamesaidia kwa kiwango kikubwa katika kukabiliana na kuenea kwa UKIMWI.

Aidha, mnamo mwaka 2007 kituo cha AMPATH-Eldoret kilianzisha huduma za mawasiliano ya rununu (simu ya mkononi) kwa wagonjwa wanaohudhuria kliniki. Huduma hii hufadhiliwa na AMPATH kwa ushirikiano wa Chuo Kikuu cha Indiana-Marekani. Baada ya mgonjwa kujisajili katika kituo hicho, anapaswa kuacha namba yake ya simu. Namba hiyo hutumika kuwasiliana na mgonjwa husika hasa kwa njia ya ujumbe mfupi, lakini wakati mwingine ikilazimu anaweza kupigiwa simu kutegemeana na ujumbe unaotarajiwa kuwasilishwa kwake. Wanaohusika hasa katika mawasiliano hayo ni wauguzi. Nilipotembelea kituo hicho niliarifiwa kuwa ujumbe huo huwa siri kati ya muuguzi na mwathirika (aghalabu mawasiliano hayo hufanyika hasa kwa Kiswahili, wakati mwingine ikilazimu lugha za mama huweza kutumika). Madhumuni hasa ya ujumbe huo ni kuwakumbusha waathirika kumeza dawa kila siku, kuhudhuria miadi bila kukosa na kuripoti kisa chochote kuhusu madhara ya dawa za ARVs alizopewa. Kwa upande mwingine waathirika wanaweza kujibu ujumbe mfupi waliopokea ikiwa wanahitajika kufanya hivyo au hata kupiga simu. Kwa mujibu wa wauguzi wanaohusika na wagonjwa, huduma hii ya mawasiliano ya simu imefaulu sana kwani waathirika wengi wameripoti kunufaika, hasa kutokana na ujumbe mfupi wanaopokea.

Kwa upande mwingine kuna huduma ya kuuliza maswali yahusuyo UKIMWI iliyozinduliwa na shirika la *One World Kenya* (OWK)[13] mnamo mwaka 2004. Huduma hiyo imewawezesha watumiaji rununu kupata usaidizi juu ya athari za UKIMWI. Mtumiaji rununu huhitajika kutuma ujumbe kwa shirika la OWK kisha kupokea majibu punde tu ujumbe wake unapopokelewa (Mwaniki, 2004). Inaaminika kuwa huduma hii ndiyo bora zaidi katika kuwahamasisha wananchi juu ya athari za UKIMWI na kukabiliana na changamoto zinazosababishwa na ugonjwa huo. Changamoto ya kwanza ni kuwa ingawa huduma hii ya kutuma na kupokea ujumbe mfupi kupitia rununu ni nzuri na tena ya haraka, shida mojawapo ya njia hii ni idadi ndogo ya maneno inayoweza kutumwa na kupokelewa kwa kila ujumbe. Pili, mtumiaji rununu anaweza kutuma na kupokea ujumbe mmoja kila siku.

## 5.0 Hitimisho

[13] Hili ni shirika linalojihusisha na vita dhidi ya UKIMWI kwa kutumia mtandao wa rununu. Kwamba waathirika wa UKIMWI huwasiliana na washauri wao ili kupata ushauri unaowawezesha kukabiliana na ugonjwa huu.

Makala haya yalilenga kubainisha nafasi ya lugha katika vita dhidi ya UKIMWI kwa kujikita katika uamilifu wa lugha. Njia tatu kuu za mawasiliano zilichunguzwa nazo ni kimaongezi, kimaandishi na kielektroniki. Kutokana na utafiti huu imebainika wazi kwamba lugha ina nafasi kubwa katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Pia nimeeleza kuwa wadau wote katika shughuli ya kuwaelimisha wanajamii juu ya UKIMWI hutumia maneno teule kutegemeana na muktadha na azma ya mawasiliano. Kwa jinsi hiyo, mafunzo juu ya kukabiliana na ugonjwa huu hatari yanaweza kutolewa kupitia mawasiliano ya maongezi, maandishi na pia elektroniki. Mbinu hizi zimebainika kuwa faafu zaidi, hasa ikizingatiwa kwamba watu mbalimbali wanaweza kufikiwa kupitia mbinu maalumu ya kimawasiliano. Kuna wale wanaopendelea mawasiliano ya maongezi, wengine ya maandishi, ilhali wengine wanafurahia ya kielektroniki. Uteuzi wa mawasiliano mwafaka hutegemea hali na miktadha ya wanajamii wanaolengwa. Kwa vyovyote vile, ni muhali kutaja kuwa njia hizi zote za mawasiliano zimetumika na zinaendelea kutumika katika kukabiliana na kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI, kwa ambavyo zinachangia sana katika kuwaelimisha wanajamii kuhusiana na janga hilo. Kwa hakika lugha ina nafasi yake maalumu katika vita dhidi ya UKIMWI.

## Marejeo


Biblia Takatifu (1997). *Methali 5:15*. Nairobi: Bible Society of Kenya.

Biblia Takatifu (1997). *Kutoka 20:17*. Nairobi: Bible Society of Kenya.

C.D.C. (2008). *Kinga ya virusi vya UKIMWI kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI.* Nairobi: M.O.H.

Entwisle, S. (2005). *Language as a social construction.* London: OUP

Githaiga, A. na wenzake (2008). *Mastering PTE: Socila Studies.* Nairobi: Oxford University Press.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, M.A.K. (1985). *Explorations in the Functions of Language*. New York: Edward Arnold, Publishers Ltd.

Kandagor, M. M. (2000). Utenzi wa Istilahi Miongoni mwa Machokoraa Nchini Kenya.

Uchunguzi wa Mtaa wa Ngara, Nairobi. Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi.

Kunhiyop. S. W. (2008). *African Christian Ethics*. Nairobi: World Alive Publishers.

Kutol, K. na wenzie (2009). ‘Role of Print Media in Conflict Management.

During the 2007/2008 Post Election Violence in Kenya: The case of the Standard and Taifa Leo Newspapers', katika *Journal of Intra African Studies*, Juzuu la 2.

Lacey, M. (2004). *For Africa Deaf and blind, Aids is unknown Language.* The New York Times.

Mutembei, A. (2009). 'Communicating AIDS Messages through Billboards and Murals in Tanzania: Redifining Swahili Literature', katika *Journal of Humanities*. Juz. 2, 2009.

Mwaniki, A. (2004). *Text Aim to fight Aids in Kenya.* Nairobi; OWK Ltd.

Ogechi, N.O. (2005). *The language of Sex and HIV/AIDS among University Students in Kenya.*

Ogechi, N. O. (2002). *Mbinu za Mawasiliano kwa Kiswahili.* Eldoret: MUP.

O'grady, W. na wenzie (1997). *Language: A preview*. In Conteporary Linguistics. Lancaster. Addison Wesley Longman Publishers Ltd.

Simala, I. K. (2008). *Nadharia na Utandawazi katika Maendeleo ya Taaluma ya Kiswahili:* Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika. Wah. Ogechi, Shitemi & Simala. Moi University Press.

Sharma, S. (2008). *Wireless & Cellular Communication*. Katson Books

Taylor, S. na wenzie. (1980). *Essence Communication*. London. Oxford University Press.

Treichiler, P. (1989). *AIDS, Homophobia and Biomedical Discource. An Epidemic of signification in Aids cultural Analysis.* Cambridge. Cambridge University Press.

Wain, S. (2005). *1959 and all that: Immunodeficiency viruses: The history of AIDS*. CNN.

Daily Nation Newspaper, 20th May 2010. *Clerics urged to join fight against Aids stigma*. NMG